# MKATABA WA KUKODISHA ENEO LA WAZI

**MAKUBALIANO** haya yamefanyika leo tarehe ....... Mwezi April, Mwaka **2024**

**KATI YA**

**HALIMASHAULI YA KIJIJI YA KWABOJO** wa S.L.P. 355 kata ya Mgambo, Wilaya ya Handeni, Tanga (ambaye hapa ataitwa ("**MWENYE ENEO LA WAZI**") neno ambalo litamjumuisha , wadau ,washirika wake na wote watakaodai haki kutokana na Mkataba huu kwa upande mmoja,

**NA**

**M/S KACHCHH MINING AND TRADING LIMITED** wa S.L.P 05 **TANGA** Kampuni iliyosajiliwa kihalali na kupewa namba ya usajili numba 168678517 na leseni ya master dealer number DL0017TNG/EZ/2023-24 yenye kujishughuilika na madini chuma hapa kijijini kwa bojo maeneo ya **HANDENI- TANGA**(ambaye anaitwa ("**MKODISHWAJI**")neno ambalo wadau wake na yeyote atakayedai haki kutokana na mkataba huu kwa upande wa pili.

**AMBAO:**

A. **KWAMBA 'MWENYE ENEO LA WAZI"** ndiye mmiliki halali wa eneo hilo lenye ukubwa wa ekari 14 liloko katika kijiji cha kwa bojo katika kata ya mgambo wilaya ya **HANDEN**I mkoa wa **TANGA**

B. **KWAMBA," MKODISHWAJI**" ametangaza kwa" **MWENYE ENEO LA WAZI"** kuwa analo uhitaji la kukodisha na kutumia kipande cha ardhi kwa ajili ya kuhifadhi madini Chuma (Iron ore) lenye ukubwa wa ekari kumi(10) na kujenga nyumba za wafanya kazi na miundo mbinu kwa ajili ya kupakia na kupakua pamoja na kuhifadhi madini chuma.

C. **KWAMBA "MKODISHIWAJI'** anafanya shughuli zake halali za madini chuma maeneo ya kijiji cha kwa bojo na kwa vile hilo eneo la linalotakiwa kukodishwa liko karibu na barabara litamwezesha kupeleka hayo madini chuma kwa urahisi na kuhifadhi hapo na kuyaondoa na kuyasafirisha mahali anapotaka.

D.**KWAMBA "MWENYE ENEO LA WAZI"** anayonia pasipo kushinikizwa amekubabali kulikodisha eneo hilo lenye ekari kumi (10)



CamScanner

CamScanner

ambazo nne zipo mbele ya barara na kumi (10) ziko nyuma kidogo ili aweze kufanya pakuhifadhia madini chuma na kutengeneza miundombinu ya kuingiza magari ya kubebea madini chuma na kushusha.

E.**KWAMBA "MKODISHWAJI"**naye anayo nia na amekubali pasipo kushinikizwa kukodi eneo hilo lenye jumla ya ekari kumi (10) ambalo limetengwa na halimashauri ya kijiji cha kwa Bojo kama eneo la wazi kwa ajili ya shughuli za kuhifadhi madini chuma ambayo atapatumia pia kama kituo cha kushusha na kupakia madini hayo na kujenga Kambi za Wafanyakazi.

**HIVYO BASI MAKUBALIANO HAYA YAMEFANYIKA KAMA IFUATAVYO:**

1. **"MWENYE ENEO LA WAZI"** amekubali kumkodisha" **MKODISHWAJI"** eneo la wazi la kijiji cha kwa Bojo kwa ajili ya kuhifadhi madini ya chuma kujenga kambi na miundo mbinu mingine kwa kazi yake kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia tarehe ya mkataba huu utakapo sainiwa.

2. **KWAMBA "MKODISHWAJI"** atamlipa **"MWENYE ENEO LA WAZI"** kodi ya kila mwezi kwa kiasi cha shilingi za Tanzania laki nne (**400,000/**) kwa mwezi na wamekubaliana pande zote mbili kua malipo yalipwe kwa miezi kumi nambili (12) yaani kwa kila mwaka kwa muda wa miaka mitano na kila mwaka tutakaa kujadili kabla ya kulipana tena mkataba huu ni miaka mitano na pia unaweza kuongezwa tena pindi tutakapokubaliana tena **MKODISHWAJ**I analipa kiasii cha shilingi millioni nne laki nane (**4,800,000/**) hivyo basi kodi hii ikilipwa mwezi huu tunaanza kuhesabu kuanzia Mwezi june na mpaka mwezi june mwakani 2025.Malipo hayo yatalipwa kwenye account ya bank ya Hlimashauli ya kijiji .

3. **KWAMBA " MKODISHWAJI"** ataruhusiwa kujenga miundombinu majengo anayo hitaji kwa ajili ya kazi yake na kama atataka kupanunua baadae atakaa na Hali mashauri ya nkijiji na kama wataridhia basi ununuzi utafanyika la sivyo kama atabaki kua **MKODISHWAJI** miundombinu atakayojenga siku akisema anaondoka atalazimika kuwaachia kijij .



CamScanner

CamScanner

4. **KWAMBA "MWENYE ENEO LA WAZI"**: hataruhusiwa kufanya shughuli yeyote kwenye hilo eneo lilikodishwa na haruhusiwi kumpangisha mtu mwingine" **MKODISHWAJI"** pia nae haruhusiwi kumkodisha mtu mwingine yeyote zaidi yeye tu, wakati wa utekelezaji wa mkataba huu.na **"MKODISHWAJI"** atawajibika kushirikiana na kijiji kwenye shughuli za ustawi wa kijiji kama vile kutoa michango mbali mbali kwa ajili ya ukjenzi wa Shule Zahanati, bwawa la maji , kisima cha maji , kwa ajili ya ustawi wa maendeleo ya kijiji kwa ujumla.

5. **KWAMBA** kama yatatokea matatizo yeyote kaatika utekelezaji wa mkataba huu, upande husika utatoa taarifa ya maandishi kwa upande mwingine juu ya matatizo yaliyojitokeza ndani ya muda muafaka na pande zote mbili zitakaa na kuamua jinsi ya kutatua hayo matatizo .

6. **KWAMBA** upande wowote kati ya **"MWENYE ENEO LA WAZI"** na **"MKODISHWAJI"** uko huru kuvunja mkataba kwa kutoa sababu za msingi na atatoa ilaani ya maandishishi ndani ya siku Thelathini (30) na upande utakaovunja utawajibika kuvunja mkataba utawajibika kulipa gharama zitakazotokana na kuvunja mkataba. Kwa kulipa sehemu ya kazi ambayo imefanyika baada ya kufanya makadirio na makubaliano ya pande zote mbili.

7. **KWAMBA** : Mkataba huu unaweza kufanyiwa marekebisho wakati wowote itakapoonekana inafaa na kwa upande unaohitaji kufanya hivyo kutoa ilaani ya maandishi kwa upande mwingine ukianisha sababu za msingi za kutaka marekebisho hayo yafanyike.

8. **KWAMBA** iwapo kutatokea mgogoro au kutoelewana kati ya pande mbili **"MWENYE ENEO LA WAZI"** na **MKODISHWAJI** Mgogoro huo utasuluhishwa kwanza kwa njia ya majidiliano na ikiwa hakutakua namaelewano basi sheria za mkataba za jamhuri ya muungano wa Tanzania zitatumika

9. **KWAMBA** :lugha itakayo tumika ni **KISWAHILI** na **KINGEREZA.**

**KWA USHUHUDA HUU MKATABA HUU UMETIWA SAINI LEO TAREHE............ MWEZI............ MWAKA....................**

CS CamScanner

CS CamScanner

**IMESAINIWA NA KUWASILISHWA NA:**

**MWENYEKITI WA KIJIJI CHA KWA BOJO:**

**JINA:** SELEMANI MOHAMEDI KISOME

**SAINI:** ......................................

**TAREHE:** 26/04/2024

**MAHALI : HANDENI/TANGA**

**AFISA MTENDAJI WA KIJIJI CHA KWA BOJO**

**JINA:** SHFIANI HOSENI ATHUMANI

**TAREHE:** 26/04/2024

**SAINI:** ......................................

**MAHALI: HANDENI/TANGA**

**MBELE YA:**

**JINA:** KOLETA J. CHIM...

**WADHIFA: MWANASHERIA**

**SAINI:** ......................................

**TAREHE:** 26/04/2024

**MAHALI:HANDENI/TANGA**

**M/S KACHCHH MINING AND TRADING LIMITED**

**JINA LA MUHUSIKA:** CHANDULAL R. SENGHANI

**SAINI:** ......................................

**TAREHE:** 26/04/2024

**MAHALI : HANDENI/TANGA**

CamScanner